# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

***Dodoma***
***15 Juni, 2025***

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema matarajio ya wananchi kwa Mahakama ya Tanzania ni kuona Mahakama hiyo inatenda haki kwa wote na kwa wakati, akisisitiza uwajibikaji na ufanisi kama nguzo kuu katika kuimarisha imani ya wananchi kwa Mhimili huo.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo leo Ikulu Chamwino katika hafla ya kumuapisha Jaji wa Mahakama ya Rufani George Mcheche Masaju kuwa Jaji Mkuu wa Tanzania.

Vilevile, Rais Dkt. Samia amesema Serikali itaendelea kushirikiana na Mahakama katika kuimarisha mifumo, miundombinu na mazingira ya utendaji kazi ili kuongeza ufanisi wa Mhimili huo wa dola.

Aidha, Rais Dkt. Samia ametoa msisitizo kwa Majaji wote kuendelea kusimamia misingi ya haki kwa uadilifu na weledi ili kuimarisha hadhi ya Mhimili huo duniani.

Katika hatua nyingine, Rais Dkt. Samia ametoa wito kwa Mahakama ya Tanzania kuendeleza utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai ili kuimarisha utawala wa sheria na utawala bora nchini.

Rais Dkt. Samia amemshukuru Jaji Mkuu Mstaafu Prof. Ibrahim Hamis Juma kwa mchango mkubwa alioutoa katika kuongoza mageuzi ya miundombinu, mifumo ya kazi na ufanisi wa utendaji ndani ya Mahakama ya Tanzania, akimtaja kama kiongozi aliyeacha alama ya kudumu katika utumishi wake ndani ya Mahakama.

Jaji Mkuu Masaju amekuwa Jaji Mkuu wa kwanza kuapishwa jijini Dodoma tangu shughuli za Mahakama kuhamia rasmi Makao Makuu ya nchi.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu